

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



**OFISI YA RAIS
TUME YA UTUMISHI WA WALIMU,**

FUNGU 002

**TAARIFA YA UTAFITI KUHUSU TATHIMINI YA
UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA TUME TANGU
KUANZISHWA KWAKE MWAKA 2016**

Imetayarishwa na:-

*Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu,
S.L.P 353,
Mtaa wa Mtendeni
DODOMA.*

Simu: 026 23224624

Tovuti: www.tsc.go.tz

Barua pepe: secretary@tsc.go.tz

NOVEMBA, 2021

YALIYOMO

TAARIFA YA UTAFITI KUHUSU TATHIMINI YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA TUME TANGU KUANZISHWA KWAKE MWAKA 2016	2
SURA YA KWANZA.....	2
1.0 Utangulizi.....	2
1.2 Dira.....	2
1.3 Dhima .. .	2
1.4 Majukumu ya Tume ya Utumishi wa Walimu.....	2
1.5 Muundo wa Tume ya Utumishi wa Walimu .. .	4
SURA YA PILI.....	7
2.0 MAFANIKIO YA TUME YALIYOPATIKANA TANGU KUANZISHWA KWAKE	7
(b) Masuala yanayohusu Ajira na Maendeleo ya Walimu.....	7
SURA YA TATU.....	18
3.0 Utangulizi.	18
3.6.2 Maeneo ya Utafiti	20
3.6.2 Sampuli ya Washiriki wa Utafiti .. .	22
3.6.4 Zana za Kukusanya Data. .. .	23
SURA YA NNE.....	24
Uwasilishaji na uchambuzi wa taarifa.....	24
SURA YA TANO	42
Matokeo ya utafiti.....	42
5.4 Hitimisho .. .	43

TAARIFA YA UTAFITI KUHUSU TATHIMINI YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA TUME TANGU KUANZISHWA KWAKE MWAKA 2016

SURA YA KWANZA

1.0 Utangulizi

1.1 Maelezo kuhusu Tume ya Utumishi wa Walimu

Tume ya Utumishi wa Walimu imeundwa kwa Sheria Na.25 ya mwaka 2015 na ilianza kufanya kazi kwa mujibu wa sheria tarehe 1/4/2016. Hata hivyo, utekelezaji wa kazi zake ulianza kupitia bajeti ya 2016/17. Tume ya Utumishi wa Walimu ni Mamlaka ya Ajira na Nidhamu kwa Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari walio kwenye Utumishi wa Umma, Tanzania Bara.

Katika kipindi cha miaka mitatu (2016/17 – 2018/19), Tume imetekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Kifungu cha 5 cha Sheria ya Utumishi wa Walimu Na. 25 ya mwaka 2015. Katika kipindi hicho, Tume iliweka vipaumbele katika usimamizi wa masuala ya Ajira na Maendeleo ya Walimu, kutoa uamuzi wa Mashauri ya Nidhamu, Rufaa na Malalamiko ya Walimu kwa mujibu wa sheria na kwa wakati.

1.2 Dira

“Taasisi inayoongoza katika kuwezesha uwajibikaji na uadilifu katika Utumishi wa Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari”.

1.3 Dhima

“Kuhakikisha walimu wa Shule za Msingi na Sekondari wanapata huduma bora kuhusu masuala ya ajira, kupandishwa vyeo na kukuza maadili”

1.4 Majukumu ya Tume ya Utumishi wa Walimu

Majukumu ya Tume ya Utumishi wa Walimu yameainishwa kwenye Kifungu Na. 5(a)–(i) cha Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Na. 25 ya Mwaka 2015 ambayo ni;

- (a) Kuendeleza na kusimamia Utumishi wa Walimu;
 - (b) Kumshauri Waziri juu ya kusimamia na kuendeleza Utumishi wa Walimu;
 - (c) Kuajiri, kupandisha vyeo na kuchukua hatua za kinidhamu kwa walimu;
 - (d) Kuhakikisha uwiano sawa katika usambazaji wa Walimu ndani ya Serikali za Mitaa na Shule;
 - (e) Kushughulikia masuala ya rufaa zinazotokana na maamuzi ya Mamlaka ya Nidhamu;
 - (f) Kutunza daftari la kumbukumbu za walimu wote waliopo kwenye Utumishi wa Umma;
- (g) Kusimamia programu za mafunzo ya walimu kazini;
- (h) Kufanya utafiti na tathmini kuhusu masuala yanayohusu utumishi wa walimu na kumshauri Waziri inavyostahiki;
- (i) Kutathmini hali ya Walimu na kushauri Wizara yenye dhamana ya masuala ya walimu juu ya mafunzo, idadi na uhitaji wa walimu nchini;
- (j) Kuandaa Kanuni za Maadili ya Utendaji kazi ya mwalimu;
- (k) Kuendeleza Mfumo wa mawasiliano na Ofisi za Tume katika ngazi ya Wilaya juu ya mambo yote au jambo lolote kuhusiana na maendeleo ya Utumishi wa walimu na kuhakikisha kwamba Mwajiri na Ofisi ya Tume ngazi ya Wilaya wanatekeleza kazi zao kwa mujibu wa Sheria;
- (l) Kufanya jambo lolote ambalo kwa maoni ya Waziri linafaa au kutegemewa katika utekelezaji bora wa kazi za Tume.

1.5 Muundo wa Tume ya Utumishi wa Walimu

Muundo wa Tume unajumuisha Idara mbili, Vitengo saba, na Ofisi katika Wilaya 139 zinazohudumia Halmashauri 184. Majukumu yote ya Tume ya Utumishi wa Walimu yanatekelezwa kwa kuzingatia Muundo wa Tume uliofanyiwa mapitio na kuidhinishwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mnamo tarehe 01 Oktoba, 2018. Muundo huu wa Tume ya Utumishi wa Walimu unaifanya kuwa na eneo kubwa inalohudumia Walimu wote nchini katika masuala ya Ajira, Kuthibitishwa kazini. Kupandishwa Vyeo, Kubadilishiwa Vyeo, kusajiriwa na kupewa namba ya TSC, Maadili na nidhamu, kusimamia Mipango ya mafunzo, kustaafu nk.

1.6 Hali ya Utoaji wa Huduma za Utumishi wa Walimu Nchini

Tume ya Utumishi wa Walimu ni Idara ya Serikali inayojitegemea (Independent Department) ilioanzishwa kwa Sheria ya Bunge Na. 25 ya Mwaka 2015. Tume ilianza kutekeleza majukumu yake rasmi tarehe 01 Julai, 2016 kupitia Ofisi zake 140 (139 ni Ofisi za Wilaya na 1 Ofisi ya Makao Makuu). Hadi kufikia tarehe 10 Agosti, 2021, Tume ina jumla ya Watumishi **523** katika ngazi ya Makao Makuu na Wilayani na wanahudumia walimu takribani **262,028** Tanzania bara ambapo wa Shule za Msingi ni **177,053** na Sekondari **84,975**.

Pamoja na ukweli kwamba hakuna utafiti au tathmini iliyowahi kufanyika hivi karibuni kuhusu hali ya Utumishi wa Walimu nchini, bado ipo imani/hisia mionganii mwa Walimu Wenyewe na baadhi ya Wadau kwamba walimu hawapati huduma bora, bado changamoto zinazohusu Utumishi wao hazijashughulikiwa ipasavyo pamoja na uwepo wa chombo ambacho kimepewa dhamana ya kuwa Mamlaka ya ajira na Nidhamu kwa Walimu waliopo kwenye Utumishi wa Umma kwa mujibu wa Sheria.

Kuendelea kuwepo kwa mtazamo na hisia za Walimu kutokutendewa ipasavyo katika masuala yao ya kiutumishi ni hatari kwa ustawi wa

kiwango na ubora wa elimu nchini, kwani walimu ni nyenzo muhimu sana katika kuboresha kiwango cha elimu nchini. Hali hii inajidhihirisha pia katika makosa ya kimaadili yanayowakabili baadhi ya Walimu waliopo katika Utumishi wa Umma. Uwepo wa vitendo vya ukosefu wa Maadili kama utoro bila sababu za msingi, wizi na udanganyifu wa mitihani, matumizi ya vyeti feki, kujihusisha na masuala ya kimapenzi na wanafunzi na kutozingatiwa kwa maadili ya kazi ya ualimu yamechangia sana katika kuporomosha nidhamu kwenye baadhi ya Shule.

Miongoni mwa sababu inayochangia uwepo wa vitendo vya ukiukwaji wa maadili na malalamiko miongoni mwa Walimu ni kiwango kidogo cha uelewa wa Sheria, Kanuni na Taratibu zinazoongoza Utumishi wao. Hata hivyo, katika kukabiliana na changamoto hiyo Tume ya Utumishi wa Walimu kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita imekuwa ikitoa elimu mbalimbali kuwahuju Walimu kuitia vipindi vya Redio na Luninga, Vipererushi na Mabango, Maenesho mbalimbali kama Nane Nane na Sabasaba, Tovuti na mitandao ya kijamii. Elimu iliyotolewa imesaidia kwa kiwango fulani kutatua changamoto ya utovu wa maadili ingawa tatizo bado ni kubwa.

Serikali pamoja na wadau wengine kwa kutambua umuhimu wa Utumishi wa Walimu kama nyezo muhimu katika kuboresha elimu nchini imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali ili kuweza kuboresha masuala yanayohusu utumishi wao. Juhudi za Serikali za kuangalia suala hili historia yake imeanza tangu nchi ilipopata uhuru miaka ya 1960 hadi sasa kwa kuanzisha mifumo ya Kisera, Kisheria na Kitaasisi kwa ajili ya kuhudumia Walimu kwa kutambua umuhimu na jukumu walilonalo la kujenga kizazi cha baadaye kwa ajili ya maendeleo endelevu ya Taifa letu. Serikali inatambua kuwa bila kuwepo kwa elimu bora uchumi na maendeleo ya Taifa hayawezi kusonga mbele.

Hata uanzishwaji wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) mwaka 2015, malengo yalikuwa ni kuongeza ufanisi katika kuwashudumia Walimu,

ambao kimsingi ni kundi kubwa ambalo huchukua zaidi ya asilimia 60 ya watumishi wa umma. TSC iliundwa baada ya iliyokuwa Idara ya Utumishi wa Walimu (TSD) chini ya Tume ya Utumishi wa Umma kuonekana kutofikia malengo ya kutoanzishwa kwake katika usimamizi wa masuala ya Walimu nchini.

SURA YA PILI

2.0 MAFANIKIO YA TUME YALIYOPATIKANA TANGU KUANZISHWA KWAKE

Katika kipindi cha miaka takribani saba iliyopita tangu ilipotungwa Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Na.25 ya mwaka 2015, na kupitishwa kwa Kanuni zake mwaka 2016, Tume imeendelea kutekeleza majukumu yake ambayo ni kuwahudumia walimu wanaofundisha Shule za Msingi na Sekondari katika utumishi wa umma Tanzania Bara.

Uongozi wa Tume kupitia agizo lilitolewa na Kamati ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa Katika kikao cha Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Utawala na Serikali za Mitaa kilichofanyika tarehe 17 Machi 2021, baada ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Mhe. Seleman Jafo kuwasilisha mapendekezo ya Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/22 mbele ya Kamati, Wajumbe wa Kamati katika kujadili na kuishauri Serikali kuhusu upande wa utekelezaji wa majukumu ya Tume ya Utumishi wa Walimu kwa kupitia kikao hicho, Wajumbe walielekeza Tume ya Utumishi wa Walimu kufanya utafiti au tathmini ya utekelezaji wa malengo ya Tume tangu ianzishwe, ili kujua iwapo imeweza kuyatekeleza kwa kiwango gani na changamoto zilizopo ili Serikali iweze kushauriwa. Pia, ipime iwapo imeweza kupunguza matatizo ya Walimu kwa kiwango gani. Katika tathmini ya utekelezaji wa majukumu ya Tume, kupitia nyaraka na taarifa za utekelezaji wa majukumu, muhtasari wa mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na:-

(a)Masuala yanayohusu Ajira na Maendeleo ya Walimu.

(i) Miongozo na Maelekezo

Kuandaa, kutoa na kufanya mapitio ya Miongozo na Nyaraka zinazohusu masuala ya Ajira na Maendeleo ya Walimu. Miongozo (format) iliandaliwa na kupelekwa kwa Kaimu Makatibu Wasaidizi wa

Wilaya zote 139. Miongozo hiyo ilihuusu Mkataba wa Ajira wa Mwalimu pamoja barua zinazohusu masuala ya ajira ambayo ni barua ya ajira, kuthibitisha kazini walimu, kubadilisha kazi/cheo walimu waliojiendeleza na vibali vya kustaafu. Aidha, ilitolewa format ya uwasilishaji wa taarifa zinazohusu masuala ya ajira. Miongozo hiyo imewezechesa kuwa na mikataba na utekelezaji wa aina moja kwa Wilaya zote.

(ii) Kuajiri Walimu

Tangu Tume ilipoanza kutekeleza majukumu yake, imeshiriki katika mchakato wa ajira unaofanywa na TAMISEMI. Jumla ya Walimu **33,522** walijiriwa kati yao, Walimu wa Shule za Msingi **19,419** na Sekondari **14,103**. Aidha, katika mwaka wa fedha 2020/21, Tume ilifanya tathmini katika Shule za Sekondari na kubaini uwepo wa upungufu wa Walimu **4,050** wa masomo ya sayansi.

(iii) Kutoa namba za Usajili wa Walimu

Tangu Tume ilipoanza kutekeleza majukumu yake imesajili Walimu **28,886** kati yao Walimu **16,783** ni wa Shule za Msingi na **12,103** ni wa Shule za Sekondari. Namba za usajili ziliwezesha Ofisi za Wilaya kuwapatia walimu hao barua za ajira za masharti ya kudumu na malipo ya pensheni. Barua hizo za ajira rasmi zimesaidia walimu kupata stahili zao ikiwa ni pamoja na kuthibishwa kazini na kupandishwa vyeo. Aidha, kati ya walimu **8,000** walioajiriwa mwezi Desemba 2020, Walimu 4,875 walisajiliwa , Walimu **2,850** wanaendelea kukamilisha taratibu za ajira ili waweze kusajiliwa, na Waariwa **144** hawakusajiliwa kwa sababu hawakuwa na sifa za ualimu.

(iv) Kuthibitisha Kazini Walimu

Katika kipindi cha miaka mitano (5) walimu **26,573** walithibitishwa kazini kati ya walimu **33,522** walioajiriwa, idadi ambayo ni sawa na **86%**.

Walimu **6,949** ambao hawakuthibitishwa walikuwa bado kwenye kipindi cha matazamio.

(v) Kupandisha cheo walimu

Katika kipindi cha miaka mitano (5) Jumla ya walimu **215,813** walipandishwa cheo kati ya walimu **219,212** waliotarajiwa. Hii ni sawa na **98%**. Aidha, walimu **41,040** walihuishiwa vyeo walivyokuwa wamepandishwa mwaka 2015/16.

(vi) Kubadilisha Kazi/ Cheo Walimu Waliojiendeleza

Tume inajukumu la kuwabadilishia kazi/cheo walimu wanaojiendeleza kutoka ngazi ya cheti kwenda Stashahada au Shahada. Katika kipindi cha 2016/17 hadi 2020/21 walimu **8,940** waliojiendeleza walibadilishwa cheo kati ya walimu **14,875** waliowasilisha maombi. Walimu 5,935 waliobaki wamekasimiwa kubadilishiwa cheo kwenye Bajeti ya mwaka 2020/21 na 2021/22.

(vii) Kushughulikia maombi ya kuajiriwa upya kwa walimu waliokuwa wamefukuzwa kazi na kuwasilisha mapendekezo kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora

Maombi ya kuajiriwa upya ya walimu **207** yalipokelewa, kuchambuliwa na kuwasilishwa kwenye Mikutano ya Tume. Hawa ni walimu waliotimiza masharti kulingana na Sheria pamoja na maelekezo ya Mamlaka. Aidha, Orodha ya walimu na maoni ya Tume viliwasilishwa kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

(viii) Kufuatilia na kuhakikisha uwiano sawa katika Upangaji na Usambazaji wa Walimu ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa na Shule

Tume imeshiriki katika mazoezi ya kuchambua na kuwapangia walimu vituo vyta kazi kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa na Shule

yaliyoratibiwa na TAMISEMI. Jumla ya walimu **33,522** waliajiriwa na kupangiwa vituo vya kazi tangu mwezi Julai, 2016 hadi Juni, 2021. Kati yao Walimu wa Shule za Msingi ni **19,419** na Sekondari ni **14,103** kama ilivyoainishwa kwenye jedwali **Na. 1**

IDADI YA WALIMU WALIOAJIRIWA				
Na.	MWAKA	MSINGI	SEKONDARI	JUMLA
1	2016/17		3,462	3,462
2	2017/18	3,636	1,043	4,679
3	2018/19	7,076	3,553	10,629
4	2019/20	103	106	209
5	2020/21	8,604	5,939	14,543
	JUMLA	19,419	14,103	33,522

(ix) Kushughulikia Mafao ya Kiinua Mgongo, Pensheni na Mirathi kwa Walimu

Tume inashughulikia mafao ya walimu waliostaifu kazi au kufariki kabla ya tarehe 1 Julai, 2004 kwa kuwa, Sheria ya Hitimisho la Kazi ya Mwaka 1999 ilikuwa haijaanza kulipa mafao. Pia, Tume inashughulikia mafao ya walimu walioajiriwa kwa mikataba ambao hawalipwi na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii badala yake hulipwa na Wizara ya Fedha na Mipango.

Katika kipindi cha miaka mitano, jumla ya majalada **2,215** ya Pensheni, Mirathi na Mikataba yalipokelewa. Majalada hayo, yalifanyiwa uchambuzi wa nyaraka, ukokotoaji wa hesabu na kuwasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na HAZINA kwa ajili ya malipo. Kati ya majalada hayo, majalada **760** yalihusu Mikataba, **151** Pensheni na **633** Mirathi. Majalada **671** yaliyokuwa yamebaki yanaendelea kushughulikiwa kwa kadri Tume inavyopokea vielelezo muhimu kutoka kwa waajiri/walimu au wasimamizi wa mirathi.

(x) Kufanya Tathmini kuhusu Hali ya Walimu na kushauri ipasavyo kuhusu Mahitaji wa Walimu

Katika kipindi cha mwaka 2016/17 hadi robo ya kwanza ya mwaka 2019/2020, Tume ilikusanya taarifa kuhusu upungufu wa walimu uliotokana na walimu kustaafuli kazi, kufariki au kufukuzwa kazi na kubaini kuwa, idadi hiyo ni kubwa ikilinganishwa na idadi ya walimu walioajiriwa. Licha ya upungufu unaotokana na kuongezeka kwa shule na ongezeko la wanafunzi, taarifa inaonesha kuwa, walimu walioondoka katika Utumishi wa Umma kwa kustaafuli kazi, kufariki au kufukuzwa kazi walifikia **24,727**. Idadi hiyo ni kubwa ikilinganishwa na idadi ya walimu **18,559** waliokuwa wameajiriwa katika kipindi hicho. Kupitia tathmini hiyo Serikali iliweza kuajiri Walimu wengine **4,549**.

(xi) Kufanya ufuutiliaji kwenye Ofisi za Wilaya kuhusu utekelezaji wa masuala ya Ajira na Maendeleo ya Walimu

Katika kipindi cha miaka mitano ufuutiliaji umekuwa ukifanyika mara kwa mara kwenye Wilaya 139, ili kuona utekelezaji wa majukumu yanayohusu masuala ya ajira kwa walimu na uzingatiaji wa Sheria, Kanuni, Miongozo na maelekezo kama yalivyotolewa. Taarifa ziliandaliwa, kuwasilishwa na kujadiliwa na Tume. Aidha, Wilaya zilipewa mrejesho na maelekezo ya kuboresha utendaji wao.

(b) Masuala yanayohusu Maadili na Nidhamu

Masuala ya Maadili na Nidhamu hushughulikiwa katika Ofisi za Tume Makao Makuu na Ofisi za Wilaya. Kwa kipindi cha miaka mitano (5), 2016/17 hadi 2020/21 yafuatayo yametekeliza:

Ngazi ya Makao Makuu:

(i) Mashauri ya Nidhamu yaliyopokelewa na kushughulikiwa.

Katika mwaka 2016/17, Tume ilipokea mashauri ya nidhamu 1,288 kutoka iliyokuwa Idara ya Utumishi wa Walimu chini ya

Tume ya Utumishi wa Umma, ambayo hayakuwa yamehitimishwa. Mashauri hayo yaliwasilishwa Makao Makuu kwa kuwa, kwa Sheria ya Utumishi wa Umma Namba 8 ya Mwaka 2002, Kamati za Wilaya za iliyokuwa Idara hazikuwa na mamlaka ya kutoa adhabu ya kufukuzwa kazi walimu. Kati ya Mashauri ya Nidhamu yaliyopokelewa, mashauri 339 yalishughulikiwa na kuhitimishwa Makao Makuu. Mashauri ya Nidhamu ya walimu 949 yalirejeshwa wilayani ili yakahitimishwe kwa kuwa Kamati za Wilaya zimepewa uwezo wa kutoa adhabu zote zilizopo kwa mujibu wa Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu ya mwaka 2015. Mashauri hayo yalihitimishwa.

(ii) Rufaa zilizokatwa Tume

Jumla ya rufaa **834** za walimu zilipokelewa katika kipindi cha mwaka 2016/17 hadi 2020/21 na kusajiliwa. Rufaa **738 (88%)** zilihitimishwa na Rufaa **96 (12%)** zilizobaki zipo katika hatua ya uchambuzi kwa kadri zilivyopokelewa na kusajiliwa.

(iii) Rufaa zilizokatwa kwa Rais.

Uamuzi wa rufaa uliotolewa na Tume ya Utumishi wa Walimu unaweza kukatiwa rufaa kwa Rais iwapo mrufani hakuridhika na uamuzi huo. Rais ndiye Mamlaka ya mwisho ya rufaa kwa walimu. Katika kipindi cha miaka mitano (5), 2016/17 hadi 2020/21, jumla ya rufaa **75** zilikatwa kwa Rais. Kati ya rufaa hizo, uamuzi wa rufaa **64** ulipokelewa. Uamuzi wa rufaa hizo ni kuwa, Rais alikubaliana na uamuzi wa Tume wa rufaa za walimu **56**; uamuzi wa Tume ultenguliwa rufaa za walimu nane **(8)**; na uamuzi wa rufaa **11** haukuwa umepokelewa wakati taarifa hii ikiandaliwa.

Jedwali Na.2: Taarifa ya Rufaa zilizokatwa kwa Rais kwa Miaka Mitano (5).

MWAKA	IDADI	UAMUZI WA TUME	UAMUZI WA RAIS	MAELEZO
2016/17	-	-	-	-
2017/18	23	Walimu 14 walifukuzwa kazi	Walimu 14 walifukuzwa kazi	Rais alikubaliana na Tume
		Mwalimu mmoja (1) alishushwa cheo	Mwalimu mmoja (1) alishushwa cheo	Rais alikubaliana na Tume
		Walimu wawili (2) walirejeshwa kazini	Walimu wawili (2) walifukuzwa kazi	Rais alitengua uamuzi wa Tume
		Walimu wawili (2) alishushwa cheo	Walimu wawili (2) alishushwa cheo	Rais alikubaliana na Tume
		Walimu wanne (4) walifukuzwa kazi	Walimu wanne (4) walifukuzwa kazi	Rais alikubaliana na Tume
		Mwalimu mmoja (1) alirudishwa kazini	Mwalimu mmoja (1) alirudishwa kazini	Rais alikubaliana na Tume
2018/19	27	Walimu 10 walifukuzwa kazi	Walimu 10 walifukuzwa kazi	Rais alikubaliana na Tume
		Walimu wane (4) walirejeshwa kazini	Walimu wane (4) walifukuzwa kazi	Rais alitengua uamuzi wa Tume
		Walimu nane (8) walifukuzwa kazi	Walimu nane (8) walifukuzwa kazi	Rais alikubaliana na Tume
		Walimu wawili (2) walirejeshwa kazini	Walimu wawili (2) walirejeshwa kazini	Rais alikubaliana na Tume
2019/20	20	Walimu 14 walifukuzwa kazi,	Walimu 14 walifukuzwa kazi.	Rais alikubaliana na uwamuzi wa Tume
		Walimu wawili (2) walirudishwa kazini	Walimu wawili (2) walifukuzwa kazi	Rais alitengua uamuzi wa Tume
		Walimu wanne (4)		Uamuzi wa Rais bado haujapokelewa
2020/21	5	Walimu watano (5) walifukuzwa kazi		Bado uamuzi haujapokelewa

(iv) Mikutano ya Tume.

Masuala ya Ajira na Maendeleo ya walimu na Maadili na Nidhamu hutolewa uamuzi kwenye mikutano ya Tume iliyopo kwa mujibu wa sheria. Tume inatakiwa kufanya Mikutano kwa kila robo mwaka na Mikutano mingine ya dharura kulingana na mahitaji. Aidha, Mikutano ya

Tume hutanguliwa na vikao vya Kamati za Tume. Kamati tatu za Tume ni Kamati ya Ajira na Maendeleo ya Walimu, Kamati ya Maadili na Nidhamu na Kamati ya Utawala, Fedha, Utafiti na Elimu.

Katika kipindi cha miaka mitano (5), 2016/17 2020/21, jumla ya Mikutano ya kisheria 25 ya Tume kati ya 20 vilivyopangwa kwa mujibu wa sheria vilifanyika.

Ngazi ya Wilaya:

(i) Mashauri ya Nidhamu yaliyopokelewa na kushughulikiwa.

Wilaya hupokea tuhuma za walimu watovu wa nidhamu kutoka kwa waajiri (Wakurugenzi wa Halmashauri za Majiji, Manispaa, Miji au Wilaya) ili kuendesha mchakato wa nidhamu. Katika kipindi cha miaka mitano (5), 2016/17 2020/21, Wilaya zilianzisha mashauri ya nidhamu **12,694**, kati yake, mashauri **10,904** yalihitimishwa kama inavyoonekana kwenye **Jedwali Na.3**

Jedwali Na. 3: Mashauri ya Nidhamu Yaliyofunguliwa na Kuhitimishwa

MWAKA	YALIYOFUNGULIWA	YALIYOHITIMISHWA	MASHAURI MAPYA	MAELEZO
2016/17	2,228	2,228	-	-
2017/18	2,535	2,535	-	-
2018/19	1,428	1,428	-	-
2019/20	2,493	2,493	-	-
2020/21	4010	2,220	1,790	Yalikuwa kwenye hatua za uchambuzi
JUMLA	12,694	10,904	1,790	

(ii) Makosa yaliyotendwa na walimu

Kati ya Mashauri ya Nidhamu **10,904** yaliyohitimishwa kwa kipindi cha miaka mitano (5), makosa yaliyotendwa na walimu yaliyojitekeza zaidi ni utoro kazini sawa na **62%**, kukiuka Maadili ya Kazi ya Ualimu sawa na **14%**; Kughushi sawa na **12%** na kuwa na uhusiano wa kimapenzi na

wanafunzi sawa na 5% na makosa mengine yameainishwa kwenye Jedwali Na.4.

AINA YA MAKOSA	2016/17	2017/18	2018/19	2019/20	2020/21	JUMLA	ASILIMA
Utoro	1,765	1,578	1,145	1,081	1140	6,709	62
Uzembe kazini	68	2	24	0	0	94	1
Mapenzi	39	63	60	88	304	554	5
Ulevi	16	8	9	17	180	230	2
Ukaidi	4	1	34	74	282	395	4
Wizi	1	4	9	0	0	14	0
Kukiuka Maadali	311	873	106	210	0	1,500	14
Kushindwa kutekeleza majukumu	0	0	31	0	0	31	0
Rushwa	0	6	0	0	0	6	0
Kusababisha hasara	8	0	10	0	0	18	0
Kughushi	16	0	0	1,023	314	1,353	12
Jumla Kuu	2,228	2,535	1,428	2,493	2,220	10,904	100

(iii) Aina za Adhabu zilizotolewa

Adhabu zinazoruhusiwa kutolewa kwa walimu zimetajwa kwenye Kanuni ya 12 ya Kanuni za Tume ya Utumishi wa Walimu za mwaka 2016. Kwa kipindi cha miaka mitano (5) adhabu zilizotolewa kwa walimu ni kama zinavyoonekana katika **Jedwali Na. 5**

Jedwali Na. 5: Adhabu zilizotolewa kwa Walimu kwa Miaka Mitano (5)

NA.	AINA YA ADHABU	2016/17	2017/18	2018/19	2019/20	2020/21	JUMLA	ASILIMA
1	Kufukuzwa kazi	1,402	1,801	843	1,395	1,673	7,114	68
2	Onyo	293	239	255	410	121	1,318	13
3	Kupunguzwa mshahara	106	91	87	236	219	739	7
4	Kusimamis ha Nyongeza	115	76	53	0	0	244	2
5	Kushushwa cheo	117	71	49	166	72	475	5
6	Karipio	42	58	41	151	80	372	4
7	Kufidia hasara	0	6	8	135	55	204	2
Jumla Kuu		2,075	2,342	1,336	2,493	2,220	10,466	100

(iv) Walimu ambao hawakupatikana na Hatia

Kwa kipindi cha miaka mitano (5), Walimu 438 kati ya 10,904 sawa na 4% hawakupatikana na hatia. Uamuzi huo ulitolewa kwa kuwa ushahidi uliotolewa haukutosheleza kuwatia hatiani.

(v) Mashauri ya Nidhamu yaliyoshughulikiwa na Wakuu Shule

Wakuu wa Shule ni Mamlaka za Nidhamu ya walimu kwenye maeneo yao. Jumla ya Mashauri ya Nidhamu ya walimu 1,187 yalianzishwa na kuhitimishwa. Adhabu zilizotolewa ni pamoja na onyo, karipio na kulipa fidia.

(vi) Rufaa zilizoshughulikiwa na Kamati ya Wilaya

Kamati za Wilaya ni Mamlaka ya Rufaa kwa uamuzi uliotolewa na Wakuu wa Shule. Rufaa zilizoshughulikiwa na kuhitimishwa ni tatu (3) ambapo walimu watatu (3) walipewa adhabu za Onyo na Karipio.

(vii) Kujengea uwezo Mamlaka zinazoshughulikia nidhamu kwa walimu

Tume iliratibu na kujengea uwezo wafuatao:

- a) Kaimu Makatibu Wasaidizi wa Wilaya 139 kuhusu mchakato wa nidhamu na rufaa kwa walimu;
- b) Watumishi wa Tume (Maafisa Ajira na Maadili) kutoka kwenye Mikoa sita (6) walijengewa uwezo kuhusu masuala ya Ajira na Maadili ya Kazi ya Ualimu; na
- c) Wajumbe wa Kamati za Wilaya 19 kutoka Mikoa ya Dodoma, Singida na Morogoro walielimishwa kuhusu kuandaa na kutoa uamuzi wa mashauri ya nidhamu.

(viii) Miongozo na Maelekezo

Idara iliandaa na kusambaza Miongozo na Maelekezo mbalimbali kwenye Ofisi za Wilaya na baadhi ya wadau kuhusu:

- a. Mwongozo wa Hatua za Nidhamu na Rufaa kwa Walimu;
- b. Kanuni za Maadili ya Kazi ya Ualimu;

- c. Mwongozo wa Uandishi wa Mihtasari ya Vikao vya Kamati za Ajira na Nidhamu;
- d. Maelekezo kuhusu Uandishi wa Taarifa za Kamati za Uchunguzi;
- e. Maelekezo kuhusu kushughulikia mashauri ya nidhamu na rufaa za walimu kwa wilaya zilizoonesha udhaifu katika kushughulikia mashauri ya nidhamu
- f. Maelekezo mahsusni katika Kushuhulikia mashauri ya Nidhamu na Rufaa za Walimu.

SURA YA TATU

3.0 Utangulizi

Mafanikio mbalimbali yaliyofikiwa na Tume ya Utumishi wa Walimu, yametokana na ushirikiano wa Tume na Wadau wote ambao wamepewa dhamana ya kuwahudumia Walimu kwa njia moja ama nyingine. Wadau muhimu waliofanikisha utoaji wa huduma kwa walimu pamoja na changamoto mbalimbali ni pamoja na Waajiri (Mamlaka za Serikali za Mitaa), Wizara ya Elimu, Vyama vya Walimu, Wadau wa Maendeleo na wadau wengine.

3.1 Malengo ya Utafiti

Lengo kuu la kufanyika kwa utafiti huu ilikuwa ni Kufanya tathmini ili kujua ni kwa kiwango gani malengo ya kuanzishwa kwa Tume yamefikiwa kama yalivyoanishwa kwenye Sheria iliyounda Tume. Malengo mahsusini ya utafiti yalikuwa ni;

- (i) Kutathmini iwapo Tume imeweza kutekeleza majukumu ya kuanzishwa kwake kwa kiwango gani;
- (ii) Kuangalia changamoto ambazo Tume ikakumbana nazo katika utekelezaji wa majukumu hayo; na
- (iii) Kuanisha mapendekezo ya namna ya kuondoa ama kupunguza changamatoto hizo.

3.2 Madhumuni ya Utafiti

Tume ya Utumishi wa Walimu tangu kuanzishwa kwake kwa Sheria Na.25 ya mwaka 2015, na kuanza kutekeleza majukumu yake mwezi Aprili, 2016 hadi sasa ni zaidi ya miaka mitano. Katika kipindi chote, Tume haijawahi kujifanyia tathmini kuona iwapo inatekeleza majukumu yake kwa ufanisi na Wadau wake wanaridhika na huduma zinazotolewa. Pia, utafiti huu umeanisha mafanikio, changamoto na mikakati thabiti ya kupunguza changamoto hizo ili kuboresha utoaji wa huduma kwa Walimu na Wadau wengine.

3.3 Eneo la Utafiti

Sehemu hii inaonesha utaratibu uliotumika katika kufanya utafiti huu, utafiti ulihuisha ukusanyaji wa taarifa kutoka kwa wahojiwa katika kada mbalimbali wakiwemo, Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari, Walimu Wakuu, Maafisa Elimu, Wakurugenzi kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wabunge, Waandishi wa habari, Makatibu Tawala wa Wilaya, Watumishi wa Tume nk. Wahojiwa hawa walitoka kwenye Mikoa ya Dodoma, Mbeya, Dar es Salaam, Tanga, Mwanza, Lindi, Kigoma na Tabora.

3.4 Maswali ya Utafiti

Maswali makuu ya utafiti katika kukusanya takwimu za msingi yalikuwa ni pamoja na:

1. Ni mafanikio gani yaliyopatikana na kwa kiwango gani?
2. Ni changamoto gani ambazo zimeathiri utekelezaji wa majukumu ya Tume?
3. Ni mikakati/mbinu gani zitumike katika kupunguza/kuondoa changamoyo hizo?
4. Nini maoni ya walimu wa Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari waliopo kwenye utumishi wa Umma na wadau wengine kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Tume.

3.5 Muundo wa Taarifa

Taarifa hii ya utafiti imegawanywa katika sehemu kuu tano (5) na kila sehemu inahusiana na sehemu nyingine. Sehemu ya kwanza inatoa utangulizi kuhusu majukumu ya Tume ya Utumishi wa Walimu kwa mujibu wa Sheria iliyoanzisha Tume. Aidha, sehemu hii ya kwanza imeanisha baadhi ya mafanikio yaliyopatikana kwa kipindi cha miaka mitano tangu Tume kuanzishwa. Sehemu ya pili ya taarifa hii ni utaratibu uliotumika katika kufanya utafiti, mapitio ya taarifa mbalimbali kuhusu utumishi wa Walimu.

Sehemu ya Tatu ni masuala muhimu yaliyotokana na utafiti wenyewe, na sehemu ya mwisho ni maoni na mapendekezo yaliyotokana na utafiti uliofanyika, ambayo yanaainisha nini kifanyike ili kuongeza ufanisi wa Tume katika kuwahudumia Walimu.

3.6 METHODOLOGIA YA UTAFITI

3.6.1 Mbinu

Utafiti huu ulishughulikia vipengele kadhaa vya huduma za Utumishi wa Walimu zinazotolewa ama kutekelezwa na Tume ya Utumishi wa Walimu, huduma hizo ni pamoja na kuwasajili walimu na kutoa barua za ajira, kuwathibitisha kazini, kupandisha vyeo, kubadilisha cheo/kazi wanaojiendeleza, kutoa vibali vya kustaa fu kazi na kuchukua hatua za kinidhamu na kutoa adhabu kwa walimu wanaopatikana na hatia za ukiukwaji wa maadili. Utafiti ulikusanya kwa mapana maoni ya walimu na wadau wengine namna ya kuboresha huduma zinazotolewa kwa walimu ili kuboresha kiwango cha elimu nchini.

Hivyo, basi ni wazi kuwa utafiti huu ulifanya tathmini ya utekelezaji wa majukumu ya Tume kwa kutumia mitazamo ya walimu ambao ndio wadau wakuu wa Tume. Pia, ultumia mbinu mseto na vyanzo mbalimbali vya kukusanya data, ambazo msingi wake ulikuwa katika mkabala wa kiidadi na mkabala wa kiubora.

3.6.2 Maeneo ya Utafiti

Utafiti huu ulifanyika kwenye Mikoa nane (**8**), ambayo ni Dodoma, Dar es salaam, Mbeya, Lindi, Mwanza, Tabora, Tanga na Kigoma. Vigezo vilivyotumika kuchagua mikoa hii ni pamoja na Uwakilishi kutoka kwa Kanda zote saba, Idadi kubwa ya Walimu katika Halmashauri husika na Ufinyu wa Bajeti iliyopo kwa ajili ya kazi. Kutoka kwenye kila Mkoa Wilaya **22** zilichaguliwa bila kujali mpangilio (**Random Selection**).

Mchanganuo wa eneo la utafiti kwa Mikoa ni kama inavyooneshwa kwenye Jedwali Na.6

Jedwali Na. 6 Mgawanyo wa eneo la Utafiti Kimkoa

NA	JINA LA KANDA	JINA LA MKOA	JINA LA WILAYA
1	Nyanda za Juu Kusini	Mbeya	1. Mbeya 2. Chunya 3. Kyela
2.	Kanda ya Kati	Dodoma	1. Kondoa 2. Dodoma 3. Mpwapwa
3.	Kanda ya Magharibi	Tabora	1. Nzega 2. Urambo
4		Kigoma	1. Kigoma 2. Kasulu 3. Ujiji
5	Kanda ya Mashariki	Dar es salaam	1. Ilala 2. Temeke
		Tanga	1. Tanga 2. Muheza
6	Kanda ya Ziwa	Mwanza	1. Nyamagana 2. Ukerewe 3. Illemela
7.	Kanda ya Kusini	Lindi	1. Kilwa 2. Lindi 3. Nachingwea 4. Ruangwa

3.6.3 Sampuli ya Washiriki wa Utafiti

Sampuli ya Utafiti ilihuisha wadau mbalimbali wakiwemo Walimu wa Shule za Msingi na Wadau mbalimbali kama ilivyochanganuliwa kwenye Jedwali Na . 7

Jedwali Na.7 Idadi ya waliohojiwa kwa kila Kundu

IDADI YA WALIOHOJIWA KWA KILA KUNDI				
Na .	KUNDI	IDADI WALIOPANGWA	IDADI WALIOHOJIWA	% ya Wahojiwa
1	Walimu Msingi na Sekondari	280	352	44.7
2	Makatibu Wasaidizi	22	16	2.0
3	Waandishi wa Habari	10	5	0.6
4	Wakurugenzi/Maafisa TAMISEMI(Wizara)	20	1	0.1
5	Wananchi wa Kawaida	140	113	14.3
6	Asasi zisizo za Kiserikali	30	10	1.3
7	LGAS- Wakurugenzi	22	11	1.4
8	Maafisaelimu	22	35	4.4
9	Maafisa Utumishi	22	19	2.4
10	Katibu Tawala wa Wilaya	22	11	1.4
11	Chama cha Walimu	5	29	3.7
12	Vyuo vya Ualimu	5	6	0.8
13	Watumishi wa Tume	40	14	1.8
14	Wakuu wa Shule	30	105	13.3
15	Wajumbe wa Kamati za Wilaya	40	30	3.8
16	Wathibiti Ubora wa Shule	10	20	2.5
17	Maafisa elimu kata	10	10	1.3
18	TIE,ADEM,IAE	10	1	0.1
JUMLA		740	788	

Idadi ya wahojiwa ilivuka lengo kutokana na mwitikio ambao ulijitokeza kwa baadhi ya wadau kujitokeza kwa wingi hasa kwa walimu ambao walikuwa na hamasa kubwa ya kutaka kuongea na maafisa kutoka Tume Makao Makuu. Waliona ni fursa ya pekee ya kutoa maoni na dukuduku walizonazo. Takwimu zilizokusanywa zinaonesha kuwa asilimia kubwa ya wahojiwa iliongozwa na Walimu kwa asilimia **57%** ambayo ni zaidi ya nusu ya wahojiwa wote.

3.6.4 Zana za Kukusanya Data

Zana kuu mbili zilitumiwa kukusanya data na taarifa katika utafiti huu, kwanza hojaji au dodoso ziligawiwa kwa Wadau Mbalimbali, Hojaji/Dodoso tano zilitumika kulingana na kundi la wahojiwa, makundi hayo yalikuwa ni Dodoso Na.1; kwa ajili ya (Wabunge, Makamishna wa Tume, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, OR –MUUUB, OR-TAMISEMI, MoEST, TIE, CWT, ADEM, TEA, IAE, Wathibiti Ubora wa Shule, TAPSHA na LGAs). Dodoso Na 2. kwa ajili ya Makatibu Wasaidizi na Wajumbe wa Kamati za Wilaya. Dodoso Na 3.kwa ajili ya Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari. Dodoso Na.4 kwa ajili ya Wananchi wa kawaida na dodoso Na. 5 kwa ajili ya Taasisi zisizokuwa za kiserikali zinazojihusisha na sekta ya elimu. Njia ya pili ilikuwa ni kupitia fomu ya majedwali, njia hii ilitumika kukusanya takwimu za upili kutoka kwenye Ofisi za Tume ngazi ya Wilaya na Makao Makuu kwa kupitia taarifa mbalimbali za utekelezaji wa majukumu ya Tume.

3.6.5 Uchambuzi wa Data

Data za kiidadi kutoka katika madodoso yakiwa ni majibu yaliyotolewa na wahojiwa ziliingizwa kwenye kompyuta kwenye programu ya SPSS. Kisha data hizo zilisafishwa na uchambuzi ulifanyika, kwa kiasi kikubwa uchambuzi ulihuisha takwimu za kiidadi na kwa kiwango fulani zilikuwa ni za kiubora ili kujua sababu za majibu yaliyokuwa yanatolewa.

3.6.6 Uwasilishaji wa Data

Data na taarifa za utafiti huu zimewasilishwa kwa njia mbalimbali yakiwemo majedwali, Mihimili na chati na maumbo ambayo yanasaidia kutoa picha ya ulinganifu wa takwimu zilizokusanywa na tafsiri zake.

SURA YA NNE

UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA ZA UTAFITI.

4.0 Utangulizi

Matokeo ya utafiti huu yamewasilishwa katika sehemu kuu mbili. Sehemu ya kwanza ni maoni na wadau waliohojiwa kuhusu masuala yanayohusu utumishi wa Walimu na huduma zinazotolewa na Tume ya Utumishi wa Walimu kwa walimu, lengo likiwa ni kujua wadau wana maoni na mtazamo gani kuhusu huduma zinazotolewa na Tume. Sehemu ya pili ilihusisha uchambuzi wa utekelezaji wa majukumu kwa kuangalia malengo ya kuanzishwa kwa Tume kwa mujibu wa Kifungu Na. 5(a) – (i) cha Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Na. 25 ya Mwaka 2015.

Katika utafiti huu, data zilizopatikana zilichambuliwa na kuhakikiwa kwa kina na uwasilishaji wa data umefanyika kimaelezo na kitakwimu, maelezo yametolewa kwa ufupi huku yakiambatanishwa na majedwali yenyе takwimu. Uchambuzi wa data ulilenga kujibu maswali ya utafiti huu katika kukamilisha malengo ya utafiti. Utafiti huu ulifanikiwa kufikia malengo yake mahsus i wakati wa ukusanyaji data zilizohusiana na utafiti kwa kuhusisha jumla ya watafitiwa 788. Uwasilishaji, Uchambuzi na Mjadala wa Data umefanyika katika sehemu zifuatazo:-

4.1 Sehemu ya kwanza: Taarifa binafsi/msingi

4.1.1 Jinsi za wahojiwa

Kama ilivyoelezwa hapo awali, jumla ya Mikoa nane **(8)** na Wilaya **22, zilihusika**. Watafitiwa **788** waliohojiwa, kati yao **461** sawa na **58.5%** walikuwa wanaume na **314** sawa na **39.9%** walikuwa wanawake wahojiwa **13** sawa na **1.6%** hawakujibu kuhusu jinsi zao. Hii inaonyesha kuwa idadi kubwa ya wahojiwa walikuwa ni wa jinsi ya kiume. Tofauti ya idadi ya waliohojiwa kati ya wanaume na wanawake inahusiana na

majukumu na nafasi ya wanawake katika jamii ambayo huwafanya wasionekane kwa wingi katika nyadhifa mbalimbali ukilinganisha na wanaume.

Jedwali Na. 8- Idadi ya waliohojiwa kwa Jinsi

JINSI	IDADI	%
Wanaume	461	58.5
Wanawake	314	39.9
Hakuna	13	1.6
Jumla	788	100

4.1.2 Umri wa wahojiwa

Utafiti huu ulijumuisha wahojiwa kutoka kwenye rika tofauti kuanzia umri chini ya miaka 25 na zaidi ya miaka 56. Waliohojiwa wenyе umri kati ya 26-45 walikuwa **529** sawa na 67.2%. Wenyе umri wa miaka **46** na zaidi walikuwa **238** sawa na 30.2% wakiwemo watu watu wazima wazee. Kundi kubwa la vijana katika utafiti huu linaweza kuhusishwa na idadi kubwa ya vijana katika idadi ya watu wa Tanzania. (Rejea Sensa ya Watu na Makazi ya Tanzania ya mwaka 2012). Kundi lingine la wahojiwa chini ya miaka 25 ni asilimia 2.6 ya wahojiwa wote.

Jedwali Na .9 Idadi ya waliohojiwa kwa umri

UMRI	IDADI	%
Chini ya 25	21	2.6
26-35	192	24.4
36-45	337	42.8
46-55	200	25.4
56 na zaidi	38	4.8
Jumla	788	100.0

4.1.3 Kiwango cha Taaluma kwa Wahojiwa

Utafiti huu ulihusisha wahojiwa waliohitimu shule za Msingi, Sekondari, Vyuo na Vyuo Vikuu. Idadi kubwa ya wahojiwa ambayo ni 310 sawa na 39.3% wana kiwango cha elimu ya shahada ya kwanza; ikifuatiwa na

Stashahada ambayo wahojiwa ni 132 sawa na 16.8%; Astashahada wakiwa 128 sawa na 16.2%; Shahada ya uzamili ni 97 sawa na 12.3% na Idadi ya chini ya waliohojiwa ni wenyе Shahada ya uzamivu ambao ni 4 sawa na 0.6%. Wengine ni waliohitimu Shule za Msingi na Sekondari wanaofikia asilimia 8% ya sampuli ya waliohojiwa.

Jedwali Na.10 Kiwango cha Taaluma kwa waliohojiwa

NGAZI YA ELIMU		NAMBA	%
Darasa la Saba	Kidato cha nne	23	2.9
	Kidato cha sita	29	3.7
	Astashahada	11	1.4
	Stashahada	128	16.2
	Shahada	132	16.8
	Stashahada ya uzamili	310	39.3
	Shahada ya uzamili	19	2.4
	Shahada ya uzamivu	97	12.3
	Hawakuonesha	4	.6
	Jumla	35	4.4
		788	100.0

4.2.1 Uelewa wa walimu wa Shule za Msingi na Sekondari kuhusu kufahamu na kutumia haki yao ya kukata rufaa ngazi ya Tume na Wilaya.

Swali hili lililenga kutaka kujua uelewa walimu na wadau wengine iwapo walimu wanatumia fursa yao kisheria ya kukata rufaa. Kati ya wahojiwa 145 waliojaza dodoso Asilimia 35.2% walisema walimu wana uelewa na wanajua kutumia haki yao ya kukata rufaa dhidi ya Mamlaka ya Nidhamu, Asilimia 30.3% walisema walimu hawajui, 8.3% hawakuwa na uhakika ikiwa walimu wanafahamu haki hiyo na waliobaki 26.2% hawakusema chochote. Takwimu zinaonesha kuwa bado hata wasimamizi wa haki za walimu walioanishwa kwenye jedwali wanaofikia karibu asilimia **64.8** wanakiri kuwa walimu hawajui haki yao ya kukataa rufaa, hao wakiwa ni wale waliojibu hapana, hawakuwa na uhakika na ambao hawakujibu kabisa. Takwimu hizi zinaonesha kuwa bado wasimamizi hawa hawajatimiza wajibu wa

kuwaelimisha na kuwajengea uwezo walimu ili waweze kujua haki yao ya kukata rufaa kwenye mamlaka zao za nidhamu wanapokuwa hawajatendewa haki katika masuala yanayohusu rufaa kuhusu masualaya nidhamu kama inavyoanishwa kwenye jedwali Na.11.

Jedwali Na.11: Ulinganifu baina ya Wadhifa wa wahojiwa na uelewa wao kuhusu Walimu kutumia haki ya kukata rufaa

	Wak uru gen zi	Maafi sa Utu mishi	Maa fisa elim u Msi ngi	Maafi saeli mu Seko ndari	Wath ibiti ubor a wa Shul e	Kat ibu Ta wal a	Ch am a cha Wal imu	Taa sisi za Elim u	Vyu o Vya Wali mu	TAMI SEMI	War atib u Elim u Kat a	Ju mla	%
Ndio	4	7	7	3	10	4	10	0	4	1	1	51	35. 2
Hapan a	3	5	7	8	4	1	10	1	1	1	3	44	30. 3
Sina Uhakik a	0	3	1	1	3	0	2	0	1	0	1	12	8.3
Hwaku jibu	4	4	5	3	3	6	7	0	0	2	4	38	26. 2
Jumla	11	19	20	15	20	11	29	1	6	4	9	14 5	10 0

4.2.2 Maoni kuhusu walimu wenye tuhuma za kinidhamu kupewa haki ya kusikilizwa na Mamlaka za Nidhamu ngazi ya Shule na Wilaya

Karibu 69.7% ya waliohojiwa walisema walimu wenye tuhuma za kinidhamu wanapewa haki ya kusikilizwa na Mamlaka ya Nidhamu ngazi ya Shule na Wilaya, 13.8% walisema hawana uhakika, 8.3% walisema haki hiyo haitolewi na 8.2% hawakujibu chochote. Hii inamaanisha kuwa idadi kubwa ya Wakurugenzi wa Halmashauri, Maafisaelimu, Taasisi za Elimu, TAMISEMI, Vyuo vya Ualimu, Maafisa Elimu Kata, Chama cha Walimu, Wathibiti Ubora wa Shule na Makatibu Tawala Wilaya wanajua kuwa haki hiyo hutolewa.

Jedwali Na.12: Uelewa wa waliohojiwa kuhusu Walimu kupewa haki ya kusikilizwa na Mamlaka za Nidahamu dhidi ya mashauri ya kinidhamu

	Wak uru gen zi	Maafi sa Utumi shi	Maaf isael imu Msin gi	Maaf isael imu Seko ndar i	Wat hibiti ubor a wa Shul e	Ka tib u Ta w al a	Ch a m a ch a W ali m u	Taa sisi za Elim u	V yu o vy a W ali m u	TA MI SE MI	War atib u Eli mu Kat a	J u m la	%
Ndiyo	8	16	19	12	14	5	15	0	4	2	6	10 1	69 .7
Hapana	2	0	0	1	1	0	6	0	1	0	1	12	8. 3
Sina Uhak ika	0	3	1	2	2	3	5	0	1	2	1	20	13 .8
Haw akuji bu	1	0	0	0	3	3	3	1	0	0	1	12	8. 3
Jumla	11	19	20	15	20	11	29	1	6	4	9	14 5	10 0

Pamoja na ukweli kuwa asilimia kubwa ya waliohojiwa asilimia 69.7 walikiri kuwa Walimu wanapewa fursa ama haki ya kusikilizwa kwa mujibu wa Sheria, lakini bado lipo tatizo kwa wasimamizi wa haki za walimu kama baadhi viongozi ambao ni Wakurugenzi kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa, maafisa elimu Sekondari, chama cha Walimu na maafisa Utumishi hawajui ama hawana uhakika iwapo Walimu wanapokuwa na mashauri ya kinidhamu wanapewa fursa ya kusikilizwa. Ni vyema waajiri na wasimamizi wa haki za Walimu wakajua na kuhakikisha walimu wanatumia haki yao hii ya msingi

4.2.3 Uhusiano uliopo baina ya Ofisi za TSC ngazi ya Wilaya na Ofisi za Wakurugenzi kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kushughulikia haki, Ustawi na Maendeleo ya Walimu.

Swali hili lilitaka kuona mahusiano yaliyopo katika kushughulikia masuala yanayohusu ajira, kupandishwa vyeo, kubadilishiwa vyeo na kushughulikia masuala ya kinidhamu.

Takribani asilimia 64.1% ya waliohojiwa walisema mahusiano baina ya Ofisi za TSC ngazi ya Wilaya na Ofisi za Wakurugenzi kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kushughulikia haki, Ustawi na Maendeleo ya Walimu ni mazuri , asilimi 11.0% walisema ni ya wastani, asilimia 9.7% walisema uhusiano ni mbaya wakati asilimia 15.2% hawakujibu chochote.

